


# Msimu wa Korosho mwaka 2018/19: **Mabadiliko ya Tabia au Marekebisho ya Bei?**

Shakti Pal, Origin Development Manager, Caro Nuts

7th November, 2019, Tanzania

# Korosho mwaka 2017 - Kilele cha kutokuwa na uhakika




+/-

50%

**Source**: Krishnan G. Nair, Feb WCC 2017

# Mwaka 2018 – Ilitarajiwa, lakini kwa njia zisizotarajiwa

HAITABIRIKI

Kihistoria

Haiaminiki

Ubora; bei

Kamwe tena

Anga ndio kikomo

Mwishowe, ahsante

Somo limeeleweka

_ _ _ _ _EW
C A S H

Mwenendo wa sera??

Upuuzaji

Mbali na urekebishaji wa bei

Wakati wa usindikaji wa Kiafrika

Mwenendo wa biashara usiyokuwa na uhakika

**Source**: Stakeholders view

# Marekebisho ya bei tu au mafunzo ya maana kwa wadau?




**Source**: CashewInfo, N'Kalo,

# Watangazaji Wetu...

## Mr. Stephen Quyen Tang

LongSon



Stephen Quyen Tang amepata uzoefu wa miaka mingi katika biashara ya korosho. Akiwa anaongoza ununuzi wa korosho za Kiafrika kwa ajili ya kampuni ya Long Son (mmoja wa wasindikaji wakubwa wa korosho nchini Vietnam). Katika jukumu lake la zamani kama Msimamizi wa Uzalishaji na Meneja wa Kiwanda huko Long Son pia amepata uzoefu mkubwa katika usindikaji wa korosho.

***Atachokizungumzia:*** *Atazungumza kuhusu yale yaliyopitia katika tasnia ya korosho mwaka 2018 na matokeo yake katika tasnia ya korosho nchini Vietnam kwenye ushindani na mwendekeo unaoibuka kutokana na maathiri yake.*

ACA

# Watangazaji Wetu...

## Dr. R. K. Bhoodes - CEPCI

The Cashew Export Promotion Council of India [Sponsored by the Government of India]



Dk. R. K. Bhoodes, mwenyekiti wa CEPCI, Mhandisi wa Mitambo na mwenye MBA katika Uuzaji wa Kimataifa. Alikabidhiwa Ph.D kwa thesis yake ya 'Mpito wa Tasnia ya Korosho Ulimwenguni na Changamoto kwa India'. Amechapisha karatasi zaidi ya 20 katika tasnia ya uzalishaji wa korosho, na uuzaji. Dk. R.K. Bhoodes ndiye Mshirika anayesimamia M/s. Exports Kairali, Kollam, mshirika wa M/s. Prasanthi Group ambao ni wauzaji maarufu wa korosho.

***Atachokizungumzia:** Atazungumza kuhusu yale yaliyopitia katika tasnia ya korosho mwaka 2018 na matokeo yake katika tasnia ya korosho nchini India kwenye ushindani na mwendekeo unaoibuka kutokana na maathiri yake.*

# Watangazaji Wetu...

## Mr. Wayne Tilton – Red River Foods



Wayne Tilton ni Mkurugenzi wa Afrika wa Red River Foods, amechangia sana katika ukuaji na mwendeleo wa Red River katika tasnia ya korosho barani Afrika. Alianza kazi zake nchini Ghana kwa kujitolea kupitia Peace Corps Volunteers miaka ya 2009-2011, anaendelea kufanya kazi ya kuelimisha wakulima juu ya mazoea bora. Hivi sasa anasimamia shughuli zote barani Afrika ikiwa ni pamoja na ununuzi wa karanga na kusaidia wasindikaji katika kufuata utaratibu wa usalama wa chakula. Wayne aliwahi kutumika kwenye Bodi ya Ushauri ya ACA na kwa sasa ni mwanachama wa bodi ya ComCashew.

***Atachokizungumzia:*** *Nini kilitokea Afrika mwaka 2018? Wazalishaji wanakusudia vipi kushughulikia utengenezaji wa korosho zenye ubora wa kiwango cha chini kwa sababu ya kushindwa kutumia mazoea mazuri ya kijadi yanayosababisha korosho ambazo haziuziki?*

# Watangazaji Wetu...

## Mr. Suraj Rao – *Export Trading Group*



Suraj Rao ni mtaalam wa uuzaji wa bidhaa mwenye zaidi ya miaka 18 katika sehemu kadhaa za usimamizi na uongozi katika kampuni za bidhaa. Ameshuhudia na kushiriki katika ukuaji mkubwa wa mkoa wa Afrika Magharibi kama eneo la kuuza korosho. Suraj ana ufahamu wa kina wa mnyororo wa usambazaji wa korosho na mwelekeo katika tasnia ya korosho ya Afrika Magharibi. Katika jukumu hili kama Makamu wa Pili wa Rais wa chama cha wauzaji huko Cote D'Ivoire, aliunga mkono sera nyingi za Sekta. Kwa sasa yeye ni Mdhibiti na Mkurugenzi wa Kampuni huko ETG, akiongoza biashara mbali mbali kwenye kikundi hicho.

***Atachokizungumzia:*** *Wafanyabiashara wataweza kuuza korosho zote zilizozalishwa barani Afrika au mauzo ya korosho mbichi yatazingatia ubora zaidi? Je, wanazionaje sera za biashara za korosho mbichi katika soko lenye nguvu katika mkoa huu?*

# Watangazaji Wetu...

## Mr. Gerard Klijn – TDH



Gerard amefanya kazi katika tasnia ya karanga, akilenga kukuza miradi ya korosho ya Kiafrika, kuunganisha wakulima na soko, kwa miaka 26 iliyopita. Yeye na wafanyakazi wenzake ni watu wenye shauku na imani na kati ya wale wa Uholanzi na Afrika, wote wanamsaidia awe makini wakati wote. Pamoja na washirika wa ndani, anaamini kuwa anaweza kufungua uwezo wa Kiafrika.
Pamoja na washiriki wake wa hapa hapa anaamini kwamba anaweza kufungua uwezo wa Afrika.

**Atachokizungumzia:** *Je, ni kwanini mporomoko wa soko mwaka 2018 ulikuwa tofauti kwa soko hili? Badiliko hili (la kitabia) ni la muda mrefu au ni wa muda mfupi utakaoturudisha katika hali ile ile?*